# KITENZI KISAIDIZI CHA KISWAHILI SANIFU - MTAZAMO WA SARUFI GEUZAMAUMBO ZALISHI.

Imeandikwa na:

FREDRICK MUNG'ARO BAYA

Tasnifu hii imetolewa kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Master of Arts (M.A.) katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

1993

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0146788 5
UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY
FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa na mtu yeyote kwa mahitaji ya digrii chuo kikuu kingine"

FREDRICK MUNG'ARO BAYA

(MTAHINIWA)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

KWA PROFESA LUCIA OMONDI

(Ukarimu wako   Sitausahau)

Ukurasa


| | | |
|---|---|---|
| | Yaliyomo ............................ | |
| | Shukrani ............................ | iv |
| | Vifupisho ............................ | vi |
| 1.0 | SURA YA KWANZA ........................ | 1 |
| 1.1 | Kitangulizi .......................... | 1 |
| 1.2 | Tatizo la utafiti ...................... | 2 |
| 1.3 | Upeo na mipaka ya utafiti ............. | 4 |
| 1.4 | Madhumuni ya utafiti .................. | 5 |
| 1.5 | Haipothesia ........................... | 6 |
| 1.6 | Sababu za kuchagua somo hili .......... | 6 |
| 1.7 | Yaliyoandikwa kuhusu somo hili ......... | 7 |
| 1.8 | Msingi wa nadharia .................... | 13 |
| 1.9 | Njia za utafiti ....................... | 15 |
| 2.0 | SURA YA PILI .......................... | 16 |
| 2.1 | Kundi nomino .......................... | 16 |
| 2.1.1 | Nomino ............................ | 17 |
| 2.1.2 | Kiwakilishi ........................ | 18 |
| 2.1.3 | Ngeli ............................. | 19 |
| 2.1.4 | Kivumishi ......................... | 21 |
| 2.1.5 | Kionyeshi ......................... | 23 |
| 2.1.6 | Kimilikishi ....................... | 26 |
| 2.2 | Kundi tenzi ........................ | 28 |
| 2.2.1 | KT$\longrightarrow$ TS + T + (KN, KE, KH, $\bar{S}$) .............. | 29 |
| 2.2.2 | KT$\longrightarrow$ TS + Kuwa + KN ....................... | 32 |

Ukurasa

2.2.3 KT→ TS + Kuwa + KV .......................... 34
2.2.4 KT→ TS + Kuwa na + KN ...................... 35
2.2.5 KT→ TS + Kuwa na + KN ...................... 35
2.2.6 KT→ TS + Kuwa + V .......................... 36
3.0 SURA YA TATU ................................. 37
3.0.1 Kitenzi kisaidizi (TS) ..................... 37
3.0.1.1 Njeo (nj) ................................ 38
3.0.1.2 Modali (m) ............................... 40
3.0.1.3 TS → nj .................................. 42
3.0.1.4 TS → nj + m .............................. 44
3.0.1.5 TS → nj + me ............................. 45
3.0.1.6 TS → nj + Kuwa ........................... 48
3.0.1.7 TS → nj + ki* ............................ 49
3.0.1.8 TS → nj + m + me ......................... 51
3.0.1.9 TS → nj + m + kuwa ....................... 52
3.0.1.10 TS → nj + m + ki* ....................... 52
3.0.1.11 TS → nj + m + me + kuwa + ki ............ 52
3.0.1.12 TS → nj + me + Kuwa + Ki ................ 54
3.0.1.13 TS → nj + me + kuwa ..................... 55
3.0.1.14 TS → nj + me + ki* ...................... 56
3.0.1.15 TS → nj + me + kuwa + ki ................ 57
3.0.1.16 TS → nj + kuwa + ki ..................... 58
4.0 SURA YA NNE .................................. 59
4.0.1 Utangulizi ................................. 59
4.0.1.1 Kitenzi kisaidizi katika maswali yenye viulizi ................................. 59
4.0.1.1.1 SW → KN + TS + T + (KN, KE, KH) + kiulizi.. 64

.../iii

Ukarasa

4.0.1.1.2 SW⟶ kiulizi + KN + TS + T + (KN, KE, KH) .. 64

4.0.1.1.3 SW⟶ TS + T + (KN, KE, KH) + KN ........... 65

4.0.1.1.4 Ni + Kiulizi, na kitenzi kisaidizi chenye modali .................................. 66

4.0.1.2. Kitenzi kisaidizi katika maswali yasiyo kiulizi .................................. 68

4.0.1.2.1 SW ⟶ KN + KT ........................ 69

4.0.1.2.2 SW ⟶ KT + KN ........................ 69

4.0.1.2.3 SW ⟶ M + KN + Nje + (me)+ (Kuwa) + T + (KN, KE, KH) + KN ........................ 71

4.0.1.2.4 SW ⟶ M + kuwa + nj + (me) + (ki) + T + (KN, KE, KH) + KN) ...................... 72

4.0.1.2.5 SW⟶ M + KN + Kuwa + nj + (me) + T + (KN, KE, KH) .................................. 72

5.0 SURA YA TANO ............................ 74

5.1 HITIMISHO ............................ 74

MAREJELEO - - - - - - - - - - - - - - - - - 77

## SHUKRANI

Natoa shukrani zangu kwa msimamizi wangu Profesa Mohammed Hassan Abdulaziz, Mwalimu John Hamu Habwe, Mwalimu Wamitila, Mwalimu Kineene wa Mutiso na Mwalimu Thandi. Lau si mchango wenu kazi hii isingekamilika.

Shukrani nyingi ni kwa Profesa (Bi) Lucia Omondi Ndong'a, mwenyekiti wa idara ya isimu na Lugha za kiafrika Chuo Kikuu cha Nairobi, kusingekuwa kuelewa kwako nisingemaliza kozi ya digrii ya M.A.

Ninamshukuru bwana Noah Katana Ngala ambaye mwanzoni aliniahidi udhamini wa gharama ya digrii ya pili, japo hakuheshimu ahadi yake, asingekuwa yeye nisingeanza kamwe kozi ya digrii ya pili.

Baba yangu mzazi bwana Joseph Baya yaa Baya, ninakushukuru kwa kuamua kujitesa na kujinyima ili ugharimie masomo yangu ya digrii ya pili. Mama yangu Bibi Eddah Nzingo Baya, kaka yangu na dada zangu, ninawashukuru kwa kuvumilia shida wakati matumizi karibu yote ya nyumbani yametumiwa kugharimia elimu yangu.

Ninawashukuru wote waliotoa mchango wao wa pesa ili kigharamia elimu yangu. Wengi wao siwajui wala sijawaona lakini mchango wao ulinifikia na kunisaidia. Kuhusiana na haya napenda kuwataja Silas Mwangule wa Kenya Ports Authority, Bw. William Yaa wa Port Police na Bw. Mwagona wa K.P.A. Shukrani Zingine ziwafikie Bwana na Bibi Joseph na Rachel Mujimba kwa kiwango cha pesa ambacho walinisaidia nacho.


.../v

Bw. Mungania, Kyovi John na Justine Ng'ambo msaada wa kila mmoja wenu haisahauliki maana labda isingekuwa ninyi siku fulani ningekufa njaa.

Shukurani ni kwa Bw. Stephen Kyonda, Lifti uliyonipa siwezi kuisahau. Langata toka jijini Nairobi si Karibu!

Ninawashukuru wasimamizi wa Chuo kikuu cha Nairobi kwa kuamua kunikopesha elimu baada ya kuona siwezi kuilipia mara moja.

Ninawashukuru wanadarasa wenzangu John Kamau Gatare, Mirieri, Chepkwony, Njeri, Michira, Mosoti, Mwaro na Muaka, Mchango wenu wa kitaalamu, hali na mali umenifaa sana.

Shukrani maalumu ni kwa mke wangu Esther kwa kuwa mshirika mwema wa shida na ugumu wote niliopitia.

Ninawaomba msamaha watu wote ambao niliwakera, pengine bila kudhamiria, wakati wa usomi wangu au kuombaomba kwangu. Mimi ninawasamehe wote walioniudhi, kunitesa au kunidanganya wakati wa uhitaji.

Mwisho ninamshukuru Bi Dinah K. Justus kwa kuipiga taipu vizuri kazi hii. Ninasema tena Ahsanteni nyote na ninaomba Mungu awabariki.

## VIFUPISHO NA ISHARA

| | |
|---|---|
| E | Kielezi |
| E h | Kielezi cha hali |
| E m | Kielezi cha mahali |
| E w | Kielezi cha wakati |
| H | Kihusishi |
| K E | Kundi husishi |
| Kim | Kimilikishi |
| KN | Kundi nomino |
| KV | Kundi vumishi |
| N | Nomino |
| nj | Njeo |
| O | Kionyeshi |
| S | Sentensi, SW - SWALI |
| T | Kitenzi kikuu |
| TK | Kitenzi kisoelekeza |
| TL | Kitenzi elekezi |
| TS | Kitenzi kisaidizi |
| V | Kivumishi |
| Vd | Kivumishi cha idadi |
| Vh | Kivumishi cha hali |
| Vk | Kivumishi cha kiasi |
| * | Si sahihi kisarufi |
| ⟶ | Iandike tena kuwa |
| ( ) | Kilichofungiwa kinaweza kuwepo au kisiwepo |
| [ ] | Vilivyofungiwa hutokea pamoja |
| ◯ | Kilichomo si sehemu ya sheria |

# 1.0 SURA YA KWANZA

## 1.1 KITANGULIZI

Utafiti huu ni jaribio la kufanya uchambuzi wa kimuundo na wa kisintaksi wa kitenzi kisaidizi cha kiswahili sanifu kwa kutumia nadharia ya sarufi geuzamaumbo zalishi kama ilivyoelezwa na Chomsky (1965). Tutafanya jaribio la kuchambua kitenzi kisaidizi cha kiswahili ili kubaini muundo wake na uamilifu wake.

Tutaanza kwa kutoa fasili ya dhana ya kitenzi kisaidizi. Kamusi sanifu ya isimu na lugha (1990) imeeleza kitenzi kisaidizi kama ifuatavyo:

"Katika sarufi geuzamaumbo zalishi ni kionyo kinachotawala mofimu za wakati, mofimu za hali na mofimu za nia."

Huddleston, R (1984) ameeleza kitenzi kisaidizi kama ifuatavyo:-

> Vitenzi visaidizi ni hasa vile vitenzi ambavyo hufanya kazi kama vitegemezi katika muundo wa kundi tenzi(KT), na hutofautishwa na vitenzi vikuu ambavyo hufanya kazi kama kichwa.
>
> (Tafsiri Yetu)

Lester, M. (1971:52) ametoa maelezo yafuatayo:

> Kwa maelezo sahili, kitenzi kisaidizi ni kila kitu katika sentensi toka mwisho wa kirai nomino kina-chotenda kazi ya kiima hadi mwanzo wa kitenzi kikuu. Kitenzi kisaidizi huonyesha njeo ya ama wakati uliopo au wakati uliopita, pamoja na aina mbalimbali za vitenzi vitegemezi.
>
> (Tafsiri yetu)

Fasili hizi zote zimekaribiana sana. Zote Zinakubaliana kwamba kitenzi kisaidizi ni kitenzi au ni sehemu ya kundi tenzi, na kwamba hupatikana katikati ya kiima na kitenzi kikuu. Pia fasili hizi zinakubaliana katika maelezo yake ya jukumu la kisaidizi. Fasili ya Lester (ibid) imetoa mchango muhimu kwa kuonyesha nafasi ya kimuundo ya kitenzi kisaidizi katika sentensi. Fasili hii hata hivyo imejitegemeza katika sarufi ya lugha ya kiingereza ndiyo maana imefinya njeo katika njeo ya wakati uliopo na njeo ya wakati uliopita kwa sababu hizi ndizo zinazopatikana katika lugha ya kiingereza. Kwa mujibu wa kazi hii tutatumia fasili ya kitenzi kisaidizi ifuatayo ambayo pia imejuamuisha muhtasari wa fasili zilizopo hapo juu;

> Kitenzi kisaidizi ni kiambajengo cha sentensi ambacho hupatikana katika, au kabla ya kitenzi kikuu au mzizi wa kitenzi kikuu na ambacho hufanya kazi ya kuonyesha njeo, kauli, dhamira na/au hali ya kitenzi kikuu kinachohusika.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Kiswahili kikiwa lugha ambishibainishi tofauti na kingereza ambayo ni lugha tenganishi kinaonekana katika sentensi yake kuwa na kisaidizi chenye muundo tofauti kabisa na ule wa kisaidizi cha kiingereza na lugha zingine ambazo zimeendelea zaidi na kufanyiwa utafiti mwingi zaidi, na pia uamilifu wake ni tofauti.

Katika lugha ya kiingereza kwa mfano, kuna njeo mbili tu; njeo ya wakati uliopo na njeo ya wakati uliopita. Hakuna njeo ya wakati ujao. Hii ndiyo sababu inayomfanya Lester (ibid:54) kusema yafuatayo:-

> Kwa malengo ya sarufi hii, njeo maana yake ni viambishi vya mwisho vya vitenzi vyenye kuleta mabadiliko yanayoonyesha wakati wa sasa au wakati uliopita.
>
> (Tafsiri Yetu)

Katika kiswahili njeo si viambishi vya mwisho vya vitenzi vyenye kuleta tofauti katika vitenzi hivyo kwa kuonyesha njeo ya wakati uliopo au njeo ya wakati uliopita. Fauka ya haya katika kiswahili kuna njeo ya wakati uliopo, njeo ya wakati uliopita na njeo ya wakati ujao. Nafasi ya kimuundo katika kitenzi cha kiswahili inayoonyesha njeo ni tofauti na ile ya lugha zingine kwa mfano kiingereza. Aidha katika kitenzi kisaidizi cha kiswahili kuna mofimu zinazoonyesha ukubaliano wa kiima, yambwa, nk. mofimu kama hizi hazipatikani katika kitenzi kisaidizi cha lugha zingine kama vile kiingereza. Utafiti huu basi unanuia kujaribu kuchambua kitenzi kisaidizi cha kiswahili ili kubainisha muundo wake na sheria zinazoongoza tabia yake.

Watu kadha wa kadha wamefanya uchambuzi juu ya kundi tenzi (KT) la sentensi ya kiswahili na hata pia juu ya kitenzi cha kiswahili. Hata hivyo tuna maoni yafuatayo kuhusu chambuzi hizo:

i. Chambuzi hizo hazikuwa na lengo maalumu la kushughulikia kitenzi kisaidizi kwa sababu zilidhamiria kushughulika vipashio vya sentensi ambavyo ni vipana zaidi ya kitenzi kisaidizi, hivyo basi kukitaja kitenzi kisaidizi kwa kupitia tu, au kwa kijuujuu.

ii. Nadharia zilizotumiwa kufanya baadhi ya chambuzi hizo ni tofauti na hii yetu, na baadhi ya kazi zinazopatikana kuhusu kisaidizi hazikuandikwa kwa kufuata nadharia yoyote kwa sababu waandishi hao huenda walinuia wasomaji wasiokuwa na misingi ya kiisimu au huenda hao waandishi wenyewe hawakuwa na misingi ya kiisimu.

Ujuujuu uliopo katika kazi zinazohusu kitenzi kisaidizi cha kiswahili na kutokuwepo kwa kazi zinazoonyesha kwa wazi muundo na uamilifu wa kitenzi kisaidizi hiki ndiko kulikotutia ilhamu ya kufanya uchunguzi huu.

Katika sehemu ifuatayo tutaonyesha upeo na mipaka ya utafiti wetu huu.

## 1.3 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Kiswahili kina lahaja zaidi ya kumi na nane. Lahaja hizi ni nyingi kiasi kwamba hatuwezi kushughulika kila moja yazo katika tasnifu hii moja. Kwa sababu hii tutajikita katika lahaja ya kiswahili sanifu. Sababu ya kuchagua lahaja hii ni kwamba lahaja sanifu ndiyo inayotumiwa na watu wengi zaidi katika maongezi na pia katika maandishi ikilinganishwa na lahaja nyingine za kiswahili ambazo hutumiwa na watu wachache wa maeneo fulani madogo tu. Tofauti kati ya kiswahili sanifu na lahaja nyingine ni ndogo hivyo basi kazi hii ni wakilishi na matokeo yake tunatarajia kwamba yatasaidia kuelewa lahaja yoyote ile ya kiswahili.

Kama tulivyotaja awali kazi hii itajikita katika kushughulika na muundo na uamilifu wa kitenzi kisaidizi cha kiswahili sanifu. Nadharia tutakayotumia ni ile ya sarufi geuzamaumbo zalishi. Ingawa nadharia hii imeendelezwa sana tangu iasisiwe mwaka 1957, kama tulivyokwisha kusema tutatumia nadharia hii kama

ilivyoelezwa katika Chomsky 1965.

Kwa kiasi kikubwa katika vielelezo vyetu tutatumia sentensi tendi na sahili, lakini pia tutaangalia baadhi ya mageuzi kama vile mageuzi kanushi na mageuzi ulizi.

Kwa kuwa bado hakuna ukubaliano kamili juu ya nyingi ya istilahi za isimu katika lugha ya kiswahili katika kazi hii tutatumia istilahi kama zilivyo katika Kamusi sanifu ya isimu na lugha. Pale ambapo istilahi tofauti itatumiwa tutatoa maelezo.

Baada ya kuona upeo na mipaka ya kazi hii, katika sehemu inayofuata tutaangalia madhumuni ya utafiti wetu.

## 1.4 MADHUMUNI YA UTAFITI

Utafiti huu una madhumuni yafuatayo:

i Kubaini aina za visaidizi vya kitenzi cha kiswahili ili kudhihirisha muundo wake na uamilifu wake.

ii Kuchunguza muundo wa vitenzi visaidizi hivi na kuangalia kama miundo hii ni miundo ya nje au ni miundo ya ndani; na kama ni miundo ya nje kuchunguza mabadili yanayozalisha miundo hiyo ya nje.

iii Kuchunguza kama kitenzi kisaidizi cha kiswahili ni fenomena ya kimofolojia au ni ya kisintaksia.

iv Kuchunguza ruwaza ya kitenzi kisaidizi cha Kiswahili pale ambapo kinajitokeza katika shada. Kuangalia vitenzi visaidizi vya kesi 1, 2, 3, na 4, na kubaini ni kipi katika shada hizi ni kitenzi kisaidizi na ni kipi kitenzi kikuu na kwa nini.

v. utafiti huu unadhamiria kuchunguza dhana ya njeo katika kiswahili na kuonyesha jinsi dhana hii inavyodhihirika katika Kiswahili.

Sehemu hii imeeleza madhumuni ya utafiti wetu. Sehemu inayofuata itaonyesha haipothesia zetu.

## 1.5 HAIPOTHESIA

Haipothesia za utafiti huu ni kama zifuatavyo:

i. Kitenzi kisaidizi cha kiswahili ni fenomena ya kisintaksia.

ii. Kitenzi kisaidizi cha kiswahili kinaweza kuchukua njeo, modali, aspekti ya utimilifu, aspekti ya kuendelea, na kuwa.

iii.? Kisaidizi cha kitenzi cha kiswahili kinaweza kuchambuliwa kikamilifu kwa kutumia sarufi geuzamaumbo zalishi.

## 1.6 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO HILI

Kadri tujuavyo kazi yetu ndiyo ya kwanza yenye lengo la kukichambua kitenzi kisaidizi cha sentensi ya kiswahili kwa kutumia nadharia ya sarufi geuzamaumbo zalishi. Tunatumaini kwamba kazi yetu itaziba pengo ambalo limeachwa na watafiti waliotutangulia. Kazi hii pia itatoa mchango katika hazina ya tafiti zilizofanywa juu ya lugha ya kiswahili.

Aurbach et al (1968:48) wamesema yafuatayo:

"kundi tenzi ambalo linafanya kazi ya kiarifu mara zote huwa na kitenzi kisaidizi, ......"

(Tafsiri yetu)

Tamko hili linadhihirisha kwamba kitenzi kisaidizi ni kiambajengo cha lazima katika kila sentensi. Kwa kuchambua elementi mbayo hupatikana katika kila sentensi, tunatumai kazi hii itapanua ufahamu wa sarufi ya kiswahili.

Katika sehemu inayofuata tutaangalia yale yaliyoandikwa kuhusu somo letu la utafiti.

## 1.7 YALIOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Kazi nyingi zimeandikwa juu ya sarufi ya lugha ya Kiswahili. Kundi la kwanza la wandishi ambao walishughulikia na kuandikia sarufi ya kiswahili lilikuwa la wazungu ambao waliandika ili kuwasaidia kufahamu Kiswahili wazungu wenzao ambao walikuwa wamekuja Afrika Mashariki, au ambao walidhamiria kuja eneo hili. Katika kundi hili kuna Ashton (1944), Longman (1965), Polome (1967), n.k Kundi jingine ni la wasomi ambao waliandikia sarufi ya kiswahili kwa malengo ya kitaalamu. Katika kundi hili kuna Maw (1969), Muyachina (1973), Vitale (1981), Kapinga(1983) Mdee (1986), Owili (1989), Mgullu (1990), Thandi(1988) n.k. Kundi jingine ni la wandishi ambao wameandika vitabu vya kufundishia sarufi ya Kiswahili katika shule, hasa shule za sekondari na vyuo. Katika kundi hili kuna Mbaabu (1985), Nkwera (1978), Taasisi ya elimu ya Kenya, n.k.

Ashton (Tuliyetaja), Polome (Tuliyetaja) na Loogman (Tuliyetaja) katika kazi zao waliandika juu ya karibu sarufi yote ya kiswahili. Wandishi hawa wametoa na

kuvieleza vitenzi na viambishi mbalimbali ambavyo huambishwa kwenye vitenzi. Wote wametoa maelezo juu ya njeo na aspekti. Ingawa hapana mmoja wao aliyeandika kimaalumu juu ya kitenzi kisaidizi, katika sarufi zao wameandika mengi kukihusu. Loogman ametaja vitenzi ambavyo hutumiwa pamoja na vingine ili kutoa habari zaidi kuhusu hivyo vitenzi vingine. Yeye pamoja na wale wengine wametoa mifano ya vitenzi hivi ambavyo ni modali na pia kitenzi cha kuwa. Kazi hizi zina manufaa kwetu kwa sababu zimetupa elimu ya msingi kuhusu kitenzi cha Kiswahili kwa jumla ambayo itatusaidia kukichambua kitenzi kisaidizi kwa undani.

Maw (Ibid) ameandika juu ya mahusiano ya ndani ya sentensi za kiswahili. Yeye ametumia nadharia ya Halliday katika uchambuzi wake. Katika kuzungumzia kundi tenzi, ametaja kitenzi kisaidizi. Maw (Ibid) amesema kwamba, kundi tenzi linaweza kuwa sahili au ambatani. Kundi tenzi ambatani huwa na muundo wa kisaidizi kikifuatwa na kitenzi kikuu - muudo huu ameufafanua kama TS + T. TS kwa kawaida huja kabla ya kitenzi kikuu. Baadhi ya mifano ambayo ameitoa ni kama ifuatavyo:

Hapo/ningekuwa ni /mrongo

TS / T

Ingelikuja/nikuta

TS T

Nilikuwa/na wasiwasi

TS T

Maelezo haya ni muhimu kwa uchunguzi wetu. Tutataka kuchunguza kama madai haya ni ya kweli na pia kungundua mambo mengi zaidi kuhusu kiambajengo hiki cha kitenzi kisaidizi.

Maw (Ibid) ameendelea kusema kuwa ukubaliano wa kiima katika makundi ambatani hutokea katika kisaidizi. Amesema pia kuwa azimio ~~motifu~~ la kuonyesha njeo hupatikana katika kitenzi kikuu kwenye kundi tenzi sahili, na katika kisaidizi kwenye kundi tenzi ambatani. Tunakubaliana na Maw kuhusu haya. Hata hivyo tungependa kuongeza kwamba mofimu za kuonyesha njeo, na ukubaliano wa kiima ni sehemu ya kisaidizi. Ni wazi kwamba malengo ya Maw ~~malengo yake~~ ni tofauti na yetu na ame~~fanya~~ ~~ku~~taja tu juu ya kisaidizi.

Vitale (1981) amefanya uchunguzi juu ya lugha ya kiswahili kwa kutumia nadharia ya sarufi geuzi zalishi. Ametumia nadharia ya Chomsky (1965) ; lakini pia na nyongeza fulani zilizoendelezwa na watu kama vile Bowers (1973), Fillmore (1968 a), Emonds (1970) na Chomsky (1970). Kazi ya vitale ni ya manufaa kwetu maana tutatumia nadharia sawa na yake. Nadharia yetu hata hivyo itajikita katika Chomsky (1965) bila nyongeza yoyote kama tulivyokwisha kusema.


Vitale (ibid) katika kazi yake amezungumza juu ya muundo wa sentensi ya Kiswahili Amejadili juu ya viambishi awali ambavyo vinaweza kupatikana katika kitenzi cha kiswahili Ametoa muhtasari wa viambishi hivi kama ifuatavyo;

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (kikanushi) | Kiambishi cha kiima | njeo | (kiambishi cha urejeshi) | kiambishi cha yamba | SHINA | viambishi tamati |

Kuhusu njeo amesema ifuatavyo:

> Uambishi wa kiambishi cha njeo ni wa moja kwa moja: arki ya njeo inachukuliwa kuwa sehemu ya sheria msingi za upanuzi wa KT; ...........
>
> (Tafsiri yetu)

Ametoa mfano wa kielelezo tungo kuthibitisha kauli hii kama ifuatavyo:




(Tafsiri yetu)

Ingawa vitale hakutaja neno Kisaidizi, kazi yake imegusia Kisaidizi kwa sababu njeo na viambishi awali vya kitenzi ni sehemu ya kisaidizi. Ameonyesha viambishi awali ni vipi mpangilio wake na uamilifu wa kila kimoja. Katika kielelezo tungo kilichopo hapo juu, kutoka kwenye kifundo cha KT badala ya kutumia kiambajengo sisisi NJ angetumia KS kwa sababu kiambishi cha njeo ni - li - peke yake; na mofimu -a- na - wa - zimeachwa nje bila maelezo yoyote.

Mgullu (1990) amegusia kijuujuu juu ya kisaidizi. Katika kueleza kitenzi kisoelekeza, ametoa kauli ifuatayo:

> "......kundi tenzi huanza kuambishwa kwa viambishi vingi vyenye kuwakilisha elementi mbalimbali za kisintaksia. Tunataka kugusia juu ya mpangilio wa viambishi hivi ambavyo huja chini ya kifundo cha kisaidizi."
>
> (Tafsiri yetu)

Kupitia kauli hii ameonyesha ya kuwa viambishi ambavyo huja kabla ya mzizi wa kitenzi katika kiswahili sanifu ni sehemu ya kisaidizi. Tunakubaliana na kauli hii, japo tungependa kuongeza kwamba kisaidizi cha sentensi ya kiswahili si lazima kiwe katika hali ya viambishi, wala hata si lazima kiwakilishwe na mofimu yoyote katika kitenzi cha sentensi. Mgullu (ibid) ametoa mifano mingi ya sentensi sahili za kiswahili na vielelezo tungo vyake ambamo ameonyesha kiambajengo cha kisaidizi. Mifano yake hata hivyo imefinyika tu katika kisaidizi cha aina ya viambishi awali vya kitenzi.

Owili (1989) katika tasnifu yake ya M.A ameandika juu ya kundi tenzi la sentensi ya kiswahili. Ametumia nadharia kama yetu ya sarufi geuzamaumbo zalishi. Amezungumuzia kitenzi kisaidizi na kutoa mifano ya modali za kiswahili kama vile:

Kwisha

kwenda

kupata

kuja

kuweza

kutaka, nk.

Ufafanuzi wake utatusaidia katika kazi yetu hasa juu ya uamilifu wa kitenzi Kisaidizi na ukweli mbalimbali unaotolewa na modali za kiswahili

Owili (ibid) amesema kuwa maumbo ya kiolezofaridi ya vitenzi yanaweza kutokea mawili au zaidi pamoja na yafanyapo hivyo, moja huwa kitenzi kikuu na mengine huwa kitenzi kisaidizi. Kufafanua oni hili ametoa mifano ifuatayo.

"Alikuwa angali analia"

"Nitakuwa naweza kutembea"

(Owili 1989:33)

Ameendelea kusema kuwa yaliyopigiwa mistari ndiyo maumbo ya kiolezofaridi ya vitenzi. Kwa maoni yetu vitenzi vyote viwili vilivyopigiwa msitari katika sentensi zilizopo hapo juu ni vitenzi visaidizi na hapana kimoja ambacho ni kitenzi kikuu. Tutajaribu kuthibitisha madai yetu katika

ufafanuzi.

Owili (ibid) katika kushughulikia kitenzi kisaidizi amejikita zaidi katika maana. Kazi hii itajikita zaidi katika muundo wa kitenzi kisaidizi kuliko maana ya vitenzi visaidizi hivyo.

Katika sehemu ifuatayo tutaangalia msingi wa nadharia ya utafiti huu.

## 1.8 MSINGI WA NADHARIA

Msingi wa nadharia ya kazi hii utakuwa sarufi geuzi zalishi iliyoasisiwa na Noam Chomsky katika Chomsky (1957) na kuendelezwa katika Chomsky (1965) Baadaye nadharia hii imekuja kujulikana kama nadharia standard, kwa mfano Bach(1974)ameiita hivyo. Katika sehemu hiitutatoa maelezo kwa ufupi juu ya nadharia hii.

Sarufi geuzi zalishi ni sarufi fafanuzi. Ni mfumo wa sheria ambao kwa njia ya wazi na yenye mipaka iliyo wazi huipa kila sentensi ufafanuzi wa kimuundo. Sarufi hii kwa kiasi kikubwa hushughulika na umilisi wa msemaji - msikiaji. Yaani hushughulika na mafanyiko yatokeayo akilini ambayo ni zaidi ya kile kiwango cha kuwa na fahamu, na wala sio ripoti au madai ya msemaji - msikiaji juu ya uwezo wake. Sarufi hii kwa hivyo hujaribu kueleza kile kitu maalumu ambacho msemaji anakijua.

Kulingana na sarufi geuzi zalishi, sarufi lazima iwe mfumo wa sheria ambao unaweza kuzalisha kiwango kikubwa kisicho idadi cha miundo. Mfumo huu wa sheria unaweza kuainishwa katika vijenzi vikuu vitatu vifuatavyo:


a) kijenzi cha kisintaksia

b) Kijenzi cha kifonolojia, na

c) Kijenzi cha kisemantiki

kijenzi cha kisintaksia huwa na sehemu msingi na kipashio cha mageuzi. Sehemu msingi ya kijenzi cha kisintaksia ni mfuno wa sheria ambao huzalisha seti iliyofinywa ya mikufu msingi kila mmoja ukiwa na ufafanuzi maalumu wa kimuundo unaoitwa kielelezo tungo msingi. Vielelezo tungo msingi hivi ndivyo vipashio msingi ambavyo hufanyiza umbo ndani la sentensi. Sehemu msingi pia huwa na leksikoni. Leksikoni ni seti ya maneno yasiyopangwa na yasiyokuwa katika muktadha maalumu, na sheria za uziada. Sheria hizi za uziada huongoza upangaji wa maneno ili kusiwe na urudiajirudiaji pale ambapo si lazima.

Vielelezo tungo vinavyozalishwa na sehemu msingi huchukua umbo lifuatalo:



Msamiati hutiwa katika sehemu ya chini ya michoro hii ili kuunda umbo ndani la sentensi. Kitengo cha mageuzi huwa na kanuni geuzi ambazo zinaweza kuondoa, kuongeza, kugeuza nafasi au kubadilisha umbo nje ambalo liko sahihi kisarufi na linakubalika.

Umbo nje hupewa kijenzi cha kifonolojia ambacho hudhirisha umbo nje na alama ya kuwakilisha fonetiki.

Kijenzi cha semantiki hudhihirisha fasiri ya kisemantiki ya sentensi; Yaani huhusisha muundo uliozalishwa na kijenzi cha kisintaksia na mawasilisho fulani ya kisemantiki. Katika nadharia standard, fasiri ya kisemantiki hufanywa katika kile kiwango cha umbo ndani. Katika kesi fulani hata hivyo, arki fulani za umbo nje zinaweza kuwa mwafaka katika kufanya fasiri ya kisemantiki. Ni wazi basi kwamba vijenzi vya kifonolojia na vya kisemantiki ni vya kiufasiri.

Sehemu ifuatayo itazionyesha njia tutakazotumia kufanya utafiti huu.

## 1.9 NJIA ZA UTAFITI

Sehemu kubwa ya kazi hii tutaifanya katika maktaba. Tutasoma kazi mbalimbali ambazo zimeadikwa juu ya nadharia tutakayoitumia ili kutuwezesha kuifahamu nadharia yetu kikamilifu.

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

Tutasoma pia kazi zilizoandikwa juu ya kisaidizi kwa ujumla ili tuweze kujua wazi wazi kisaidizi ni nini na jukumu lake katika sentensi. Aidha tutasoma kazi mbalimbali ambazo zimeandikwa juu ya kundi tenzi la sentensi ya kiswahili kwa ujumla, na zile zilizoandikwa juu ya kitenzi cha kiswahili na muundo wake. Kazi hizi zitatupa ujuzi wa kiujumla juu ya uwanja tunaotaka kuushungulikia. Zaidi ya hivyo yatatuwezesha kuchuja mawazo yote amabyo yatakuwa na uwezo wa kutusaidia katika utafiti wetu. Fauka ya hayo yatatuwezesha kuona yale ambayo yamekwisha kufanywa, na pia lile pengo lilioachwa ambalo tutahitajika kulijaza.

Pia tutazungumza, kujadiliana na itakapobidi kuomba ushauri kutoka kwa wataalamu wa isimu na lugha ili tuweze kupata mwongozo bora utakaotusaidia kuyafikia malengo yetu katika kazi hii.

Tutatumia pia waongezi asilia fulani wa lugha ya kiswahili kupima ikubalifu wa baadhi ya sentensi zenye shada mbalimbali za kisaidizi kwa kuuliza maoni yao.

## SURA YA PILI

## KUNDI NOMINO LA SENTENSI YA KISWAHILI

Ili tuweze kukielewa kisaidizi cha kitenzi cha sentensi ya kiswahili ni sharti kuuelewa muundo wa kundi nomino kwanza. Uhusiano wa KN and TS tutauona baadaye sheria ya KN ni kama ifuatayo:

$$KN \longrightarrow N \left( \begin{Bmatrix} V \\ KV \\ KH \\ S \end{Bmatrix} \right)$$

Kundi nomino la sentensi ya kiswahili linaweza kuwa na nomino, kiwakilishi, kivumishi, kionyeshi, kimilikishi au mchanganyiko wa mbili au zaidi ya kategoria za maneno yaliyo kwenye mabano.


2.1.1 NOMINO

KN ⟶ NOMINO

Nomino ni kichwa cha KN. Inaweza kuwa nomino au kiwahilishi. Nomino ni neno linalotaja mtu maalumu, mahali, kitu au hali. Nomino inaweza kuwa neno moja au maneno zaidi ya moja.
Kwa mfano:

NOMINO ⟶ Hamisi, Juma, Nairobi, Kisumu
Chuo kikuu cha Kenyatta, Mwalimu
mkuu, Urembo, Ujeuri, n.k.

Nomino huwa ndicho kichwa cha kundi nomino. Nomino inaweza kutumika peke yake katika kundi nomino au ikafuatwa na maneno ya kategoria nyingine.




2.1.2. Kiwakilishi


Kiwakilishi ———————— Mimi, wewe, yeye, sisi, ninyi, wao, kionyeshi, kimilikis kivumishi

Kiwakilishi ni neno ambalo hutumika badala ya nomino. Kuna viwakilishi aina mbalimbali; aina ya kwanza ni vikwakilishi nafsi. Viwakilishi hivi ni kama vifuatavyo.

| Umoja | Wingi |
| --- | --- |
| mimi | sisi |
| wewe | ninyi |
| yeye | wao |

Aina nyingine za viwakilishi ni vionyeshi, vimilikishi na vivumishi. Ingawa kateria hizi za maneno hufanya kazi maalumu katika sarufi pia hufanya kazi kama

viwakilishi. viwakilishi hivi tutavijadili hapo chini. Kifuatacho ni kielelezo tungo kuongesha nafasi ya kiwakilishi.




2.1.3 Ngeli

Kabla ya kushughulikia vivumimshi n.k. kwanza tutaangalia ngeli za nomino za kiswahili na viambishi mbalimbali ambavyo hutumika kuwakilisha ngeli hizi. Nomino za kiswahili zinaweza kupigwa mafungu katika ngeli kumi na sita. Kila ngeli huwa mafungu maalum ambazo hufanya kazi kama viambishi vya ngeli, viambishi vya kiima na viambishi vya yambwa. Kifuatacho

ni kielelezo cha kuonyesha ngeli hizi na mofimu zote tulizotaja:

| Ngeli | Kitambulishi cha nomino | Kitambulishi cha kiima | Kitambulishi cha yambwa | Kitambulishi cha urejeshi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | mu | Nafsi 1 ni | Nafsi 1 ni | ye |
| | | Nafsi 2 u | Nafsi 2 ku | |
| | | Nafsi 3 a | Nafsi 3 m | |
| 2 | wa | Nafsi 1 Tu | Nafsi 1 tu | O |
| | | Nafsi 2 m | Nafsi 2 wa | |
| | | Nafsi 3 wa | Nafsi 3 wa | |
| 3 | mu | u | u | o |
| 4 | mi | i | i | yo |
| 5 | Ji-Q | li | li | lo |
| 6 | ma | ya | ya | yo |
| 7 | ki | ki | ki | cho |
| 8 | vi | vi. | vi | vyo |
| 9 | N | i | i | yo |
| 10 | N | zi | zi | zo |
| 11 | U | u | u | o |
| 10a | N | Zi | Zi | zo |
| 11a | U | U | U | o |
| 6a | ma | ya | ya | yo |
| 15 | pa | pa | pa | po |
| 16 | ku | ku | ku | ku |
| 18 | mu | mu | mu | mo |

Viambishi hivi kama tutakavyoona baadaye hutumiwa kutambulisha ukubaliano katika vitenzi na/au vivumishi. Vitambulishi vya nomino, kiima, yambwa na urejeshi huambishwa kwenye vitenzi na vitambulishi vya nomino huambishwa kwenye mizizi ya vivumishi, viwakilishi na vionyeshi.

### 2.1.4 KIVUMISHI

Katika sarufi kivumishi ni kipashio ambacho hutoa maelezo zaidi kuhusu nomino. Kuna vivumishi ambavyo huonyesha hali; kwa mfano.

-zuri; -baya -fupi, -refu, -eusi, -eupe
-dogo -kubwa -safi, -chafu,..........

Kivumishi aina hii huchukua kiambishi cha ngeli ya nomino kinayoivumisha.

Kuna vivumishi ambavyo huonyesha idadi, na mara nyingine huitwa viidadi. Mifano yake ni kama ifuatavyo;


-moja -wili -tatu -nne -tano
sita saba nane tisa kumi
.......

Mzizi wa kiidadi huambishwa na kiambishi cha ngeli ya nomino kinayovumisha. Sita, saba, tisa na kumi havichukui viambishi vya ngeli.


Kuna aina nyingine ya vivumishi ambavyo huonyesha kiasi Mifano ya vivumishi vya kiasi ni kama ifuatavyo;

baadhi, -chache, -ingi, -ote,
fulani, kila, -o-ote

Kivumishi huja baada ya nomino kwa mfano:





Kivumishi kinaweza kutumika peke yake katika KN. Kivumishi aina hii huwa kinafanya kazi ya kuwakilisha nomino. Mfano ni kama ifuatavyo:



vitatu / saba / baadhi — vilipotea / walikufa / zilionekana

Kivumishi kinapotumika peke yake nomino huwa iko lakini imedondoshwa

Ingawa katika sura ya kwanza tulidai kwamba tutajikita tu katika sentensi sahili, hapa natuone sentensi ambayo si sahili, lakini ambayo itatusaidia kufahamu kivumishi vizuri zaidi. Kivumishi kinaweza kutumiwa kama kibainishi. Katika mazingira kama haya kivumishi huja kabla ya nomino kwa kutumia 'a' unganifu.




2.1.5 KIONYESHI

Kionyeshi ni kipashio kinachorejea kwenye muktadha wa

mahali alipo msemaji. Katika kiswahili kuna vionyeshi vya karibu, vionyeshi vya mbali na vionyeshi vya urejezi.

kionyeshi cha karibu     hi-

kionyeshi cha mbali     -le

kionyeshi cha urejezi     hi-o

Kionyeshi cha karibu huanza na mzizi hi- ambao hufuatwa na kiambishi cha kiima cha nomino inayohusika, Kionyeshi cha mbali huwa na mzizi-"le" ambao hutanguliwa na kiambishi cha kiima cha nomino inayohusika. Kionyeshi cha urejezi huwa na mzizi hi-o Katika ya mzizi huu huambishwa kiambishi cha kiima cha nomino inayohusika.

Nomino za ngeli za kwanza, pili huchukua vionyeshi tofauti kama vifuatavyo:

| ngeli | 1 | 2 |
|---|---|---|
| Kionyeshi cha karibu | huyu | hawa |
| Kionyeshi cha mbali | yule | wale |
| Kionyeshi cha urejezi | huyo | hao |

Mifano ya vionyeshi ni kama ifuatavyo:

Kiti hiki


Kiti kile

Kiti hikio → hikyo → hicho


nyumba hii

nyumba hiyo

Kionyeshi kinaweza kuja baada ya nomino kwa mfano;





Kionyeshi kinaweza kutumika kama kibainishi; kikawa kabla ya nomino kwa mfano:



Ubadilishanaji nafasi kama huu wa nomino na kionyeshi hutegemea umulikaji(Focus).

Kionyeshi kinaweza kuwa rekee bila nomino katika KN. Kionyeshi kama hiki huwa kinafanya kazi ya kiwakilishi. Kionyeshi kinapotumika peke yake, nomino huwa iko, lakini imedondoshwa.





## 2.1.6 KIMILIKISHI

Kimilikishi ni neno ambalo huonyesha uhusiano wa kitu au mtu na mwenye kumiliki kitu hicho. Kimilikishi hutegemea nafsi ya mtu anayehusika. Tazama kielelezo kifuatacho:


| | Umoja | wingi |
|---|---|---|
| Nafsi ya kwanza | -angu | -etu |
| " " pili | -ako | -enu |
| " " tatu | -ke | -ao |

Mizizi ya vimilikishi imeonyeshwa hapo juu. Mizizi hii huambishwa nyuma na viambishi vya viima vya nomino zinazomilikiwa. Kimilikishi kinaweza kutumiwa peke yake

katika KN Hapa nomino huwa imedondoshwa.




Kimilikishi kinaweza kutumiwa pamoja na nomino kwa mfano:





Kundi nomino linaweza kuwa na muundo ufuatao

$$KN \longrightarrow N + \overbrace{O + Kim + Vd + vh + vk}^{KV}$$

Kwa mfano:

Vitabu vile vyangu viwili vizuri sana




Kundi vumishi linaweza kuwa na kivumishi kimoja ali likawa na baadhi ya vivumishi vikitumiwa pamoja kama ilivyo hapo juu. Kwa sababu tumesema tutashughulikia sentensi sahili tu, hatutazungumzia kundi nomino lenye nomino na sentensi kwa sababu kundi nomino aina hii huwa si la sentensi sahili.

## 2.2 Kundi tenzi la sentensi ya kiswahili

Kitenzi kisaidizi hupatikana katika KT. kwa sababu kiswahili ni lugha ambishibainishi, arki za kitenzi kisaidizi isipokuwa modali tu huambishwa kwenye kitenzi hivyo basi si rahisi kutenga TS kutoka T, kwa sababu hii tutazalisha TS kutoka kifundo cha KT. Kwa sababu TS huzalishwa kutoka kifundo cha KT, kabla ya kujikita katika TS tutali-angalia KT kwa ujumla. Sheria ambayo inaonyesha muundo wa KT ni kama ifuatavyo:

$$\text{KT} \rightarrow \text{TS} + \left\{ \begin{array}{l} \text{T} + (\text{KN, KE, KH, } \bar{\text{S}}) \\ \text{Kuwa} + \left\{ \begin{array}{l} \text{KN} \\ \text{KV} \\ \text{KE} \end{array} \right\} \\ \text{Kuwa na} + \left\{ \begin{array}{l} \text{KN} \\ \text{V} \end{array} \right\} \end{array} \right\}$$

Sheria hii inasema kwamba huwa na mundo wa kitenzi kisaidizi cha lazima kikifuatwa na kitenzi kikuu ambacho kinaweza kufuatwa na kundi nomino, au kundi elezi, au kundi husishi, au sentensi. Kitenzi kisaidizi cha lazima pia kinaweza kufuatwa na kitenzi cha kuwa kikifuatwa na kundi nomino au kundi vumishi au kundi elezi. Kitenzi kisaidizi kadhalika kinaweza kufuatwa na kitenzi cha 'kuwa na' kifuatwa na kundi nomino au kivumishi. Sheria hii inaonyesha kuwa kundi tenzi lina ruwaza sita zifuatazo:

$$\text{KT} \rightarrow \text{TS} + \text{T} + (\text{KN, KE, KH, } \bar{\text{S}})$$
$$\text{KT} \rightarrow \text{TS} + \text{Kuwa} + \text{KN}$$
$$\text{KT} \rightarrow \text{TS} + \text{Kuwa} + \text{KV}$$
$$\text{KT} \rightarrow \text{TS} + \text{Kuwa} + \text{KE}$$
$$\text{KT} \rightarrow \text{TS} + \text{Kuwa na} + \text{KN}$$
$$\text{KT} \rightarrow \text{TS} + \text{Kuwa na} + \text{V}$$

2.2.1 $\text{KT} \rightarrow \text{TS} + \text{T} + (\text{KN, KE, KH, } \bar{\text{S}})$

Sheria hii inasema kuwa kundi tenzi lina muundo wa kitenzi kisaidizi kikifuatwa na kitenzi kikuu kikifuatwa

na kitenzi kikuu kikifuatwa na kundi nomino au kundi elezi au kundi hisishi au sentensi. Kitenzi kisaidizi tutakieleza baadaye. Kitenzi kikuu kwa mujibu wa sheria hii ni kitenzi chochote isipokuwa kitenzi cha kuwa, kitenzi cha kuwa na, na modali. Sheria ambayo inaonyesha muundo wa T ni kama ifuatavyo:

$$T \longrightarrow \left\{ \begin{array}{l} \left\{ \begin{array}{l} TK \\ TL + KN + (KV) + (KH) \end{array} \right\} + KE \\ \\ T + \bar{S} \end{array} \right\}$$


Sheria hii inasema T kinaweza kuwa na muundo wa kitenzi kisoelekeza kikifuatwa na kundi elezi; au kitenzi elekezi kikifuatwa na nomino ambayo inaweza kufuatwa na kundi vumishi ambalo linaweza kufuatwa na kundi hisishi likifuatwa na kundi elezi; au kitenzi kikifuatwa na sentensi. Kwa sababu upeo wetu ni sentensi sahili tu, hatutaangalia muundo wenye kitenzi na sentensi kwa sababu muundo huu ni wa sentensi changamano wala si sahili.

Kitenzi kisoelekeza ni kitenzi ambacho huonyesha kitendo au tukio ambacho hakihitaji urejelezi wa yambwa. Kwa mfano:

Kuja, cheka, kufa, lala, lia, amka. Kitenzi elekezi ni kitenzi ambacho kinapotumiwa huhitaji yambwa ambayo hukijaliza. Kwa mfano:


ona, tengeneza, chukua, jua, piga, weka, ficha
toa, .........

Kitenzi kisoelekeza huwa hakihitaji kijalizo. kina weza kufuatwa na kundi elezi. kundi elezi linaweza kuwa na kielezi cha hali na/au wakati kwa mfano:





Mifano zaidi ni katika sentenzi zifuatazo:

1.




2.



TS EW EM

3. Mgonjwa alikufa jana hospitalini

KN nj TK KE

N

Mifano hii inaonyesha wazi kuwa KE linaweza kuwa na kielezi cha wakati au cha hali, na KE hili linaweza kuwa na KH ndani yake. Aidha KE linaweza kuwa na N, V na H.

Kitenzi elekezi hufuatwa na kundi nomino ambalo hufanya kazi kama yambwa. Yambwa hii huwa ni kijalizo. Kundi nomino hili linaweza kufuatwa na kundi vumishi ambalo linaweza kufuatwa na kundi husishi ambalo pia linaweza kufuatwa na kundi elezi. Mifano ni kama ifuatavyo:

TS N V EM Eh

4. Juma alificha chakula kingi jikoni vizuri

KN nj Tl KN KE

N N

5. TS N kim

Fundi ametengeneza saa yangu

KN me Tl KN

N

2.2.2. KT ⟶ TS + kuwa + KN

Kitenzi cha kuwa ni aina maalumu ya kitenzi ambacho kinaweza kujitokeza katika sura tofautitofauti. Sura hizi ni:

kuwa

ni


Si/Si—

ndi—

Katika ruwaza hii ya sentensi, kundi tenzi huwa na kitenzi kisaidizi, kuwa na KN. KN katika mazingira haya hufanya kazi kama kijalizo. Mifano ni kama ifuatavyo.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6 | Mama | alikuwa | mgonjwa |
| | KN | nj kuwa | KN |
| | N | | N |
| 7. | Kadzo | ni | mwalimu |
| | KN | kuwa | KN |
| | N | | N |
| 8. | Dama | si | mwanasheria |
| | KN | kuwa | KN |
| | N | | N |
| 9. | Mulei | hakuwa | mwizi |
| | KN | kuwa | KN |
| | N | | N |

Katika mifano 7, 8, 9 kisaidizi ambacho ni njeo kinapatikana katika kuwa. Kwa mfuano katika sentensi 7 njeo inapatikana katika 'ni' ambayo inaonyesha kuwa ni njeo ya wakati uliopo. Kielelezo tungo cha kudhihirisha haya ni kama kifuatavyo.




⟹ Kadzo ni mwalimu

2.2.3 KT ⟶ TS + kuwa + KV

Sheria hii inatoa ruwaza ya sentensi ambapo kundi tenzi muundo wake ni kitenzi kisaidizi kikifuatwa na kuwa ikifuatiwa na kivumishi. Kivumishi hapa hufanya kazi kama kundi nomino la sentensi tuliyoijadili hapo juu. Kivumishi hiki hufanya kazi ya kijalizo. Mifano ni kama ifuatavyo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Vh | Vk |
| 10 | Juma | atakuwa | mwerevu | sana |
| | KN<br>N | nj kuwa | KV | |
| | | | Vh | Vk |
| 11. | Chungwa | lilikuwa | tamu | kidogo |
| | KN<br>N | nj kuwa | KV | |

2.2.4. KT ⟶ TS + kuwa + E

Sheria hii inatoa muundo wa kundi tenzi wa kisaidizi kikifuatwa na kuwa kikifuatwa na kielezi cha mahali. Katika muundo huu kielezi cha mahali hufanya kazi sawa na nomino na kivumishi tulivyovieleza hapo juu. Mifano ya muundo huu ni kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 12. | Dada | alikuwa | kanisani |
| | KN | nj kuwa | EM |
| | N | | |
| 13. | Mzee | yu | gerezani |
| | KN | kuwa | EM |
| | N | | |

Mbali na kielezi cha mahali kielezi cha hali pia kinaweza kutumika katika mazingirahayo hayo. Kwa mfano:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 14. | Dereva | alikuwa | hatarini |
| | KN | nj kuwa | Eh |
| | N | | |
| 15. | Baba | amekuwa | shidani |
| | KN | nj kuwa | Eh |
| | N | | |

2.2.5 KT ⟶ TS + kuwa + na + KN

Sheria hii inasema kuwa kundi linaweza kuwa na muundo wa kitenzi kikifuatwa na kuwa ikifuatwa na na

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

kikifuatwa na kundi nomino. Kundi nomino hili hufanya kazi kama yambwa ambayo pia huwa ni kijalizo kama ilivyo katika mifano ya hapo juu. Kitenzi hiki cha kuwa na huonyesha hali ya kumiliki au kuwa pamoja na. Mifano ni kama ifatavyo:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 16. | mwalimu | alikuwa | na | kitabu |
| | KN | nj kuwa | na | KN |
| | N | | | N |
| 17. | Askari | walikuwa | na | bunduki |
| | KN | nj kuwa | na | KN |
| | N | | | N |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 18. | Kazungu | ana | kahindi |
| | KN | kuwa na | KN |
| | N | | N |

2.2.6 KT ⟶ TS + kuwa + na + V


Sheria hii inasema kuwa kundi tenzi linaweza kuwa na muundo wa kisaidizi kikifuatwa na kuwa, ikifuatwa na na, ikifuatwa na kivumishi. Uamilifu wa kivumishi hiki ni sawa na ule wa kundi nomino ambalo tumelizungumizia hapo juu. Mifano ni kama ifuatavyo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 19. | Yohana | alikuwa | na | kizuri |
| | KN | nj kuwa | na | V |
| | N | | | |

20. Ayubu hana mirefu

KN kuwa na V

Katika muundo huu kivumishi ni sehemu ya kundi nomino ambalo nomino yake imedondolewa na sheria ya undondoshi. Kwa mfano sentensi 19 ina muundo ufuataoː




3.0 SURA YA TATU

3.0.1 Kitenzi kisaidizi (TS)

Tumetaja awali juu ya kitenzi kisaidizi bila kukifafanua. Sasa tutashughulikia kitenzi hiki tuone muundo wake na uaminilifu wake. Kama ambavyo tumekwisha kuona kitenzi kisaidizi hupatikana katika kila sentensi. Muundo wa kitenzi kisaidizi ni kama ufuatavyo:

Ks $\longrightarrow$ njeo + (modali) + (me) + (kuwa) + (ki)

Sheria hii inasema kuwa kitenzi kisaidizi huwa na muundo wa njeo ambayo inaweza kufuatwa na modali ambayo inaweza kufuatwa na me kifuatwa na kuwa ambayo inaweza kufuatwa na ki.

3.0.1.1 Njeo

Katika lugha ya kiswahili kuna njeo tatu. Njeo hizi ni, njeo ya wakati uliopita, njeo ya wakati uliopo na njeo ya wakati ujao. Kati ya njeo tatu ni mbili tu ambazo zina viambishi maalumu kuzionyesha. Njeo hizi ni njeo ya wakati uliopita mbayo huonyeshwa kwa kiambishi li, na njeo ya wakati ujao ambayo huonyeshwa kwa kiambishi ta. Viambishi a, na, na, me hutumiwa kuonyesha njeo na pia aspekti kwa wakati huo huo mmoja.

Kiambishi -a- kwa mfano katika kitenzi "aimba" huonyesha njeo ya wakati uliopo. Kiambishi hiki pia huonysha aspekti ya tabia au hali ya kawaida ya mtenda kufanya kitendo hicho. Aspekti hii inaweza kupatikana katika mazingira ya sentensi ifuatayo:

21. Juma aimba tangu mwaka jana.

Kiambishi hiki -a- katika sentensi hii kinaonyesha kwamba Juma anaimba sasa, lakini pia amekuwa akiimba tangu mwaka jana.

Kiambishi -na- hutumiwa kuonyesha njeo ya wakati uliopo. Kwa wakati huo huo kiambishi hiki huonyesha aspekti ya kuendeleo kufanyika kwa kitendo au tukio linalohusika.

Kiambishi -me- hutumiwa kuonyesha aspekti ya kukamilika kwa kitendo au tukio linalohusika. Kiambishi hiki pia hutumiwa kuonyesha njeo ya wakati uliopita.

Viambishi hu- na -ki- ni viambishi ambavyo huonyesha aspekti tu. Kiambishi hu- huonyesha urudiaji wa kidesturi wa kitendo au tukio linalohusika. Wakati kiambishi hiki kinapotumiwa kitenzi huwa hakichukui viambishi vingine vyovyote·Kwa mfano.

22. Juma huimba
23. Hamisi hucheza mpira
24. Simba hula nyama

Kiambishi -ki- hutumiwa kuonyesha aspekti ya kufanyika kwa kitendo au kutukia kwa tukio. Aspekti hii haifungwi na njeo; Inaweza kuwa katika mazingira ya njeo ya wakati uliopita, au wakati ujao au wakati uliopo. Kwa mfano:

25. Hadija alikuwa akipanda mnazi alipoanguka.
26. Dhababu atakuwa akisoma nitakapofika
27. Amina anaonekana akicheka kitandani.

Kiambishi -ka- hutumiwa kutambulisha aspekti ya tukio linalotukia au kitendo kinachofanyika baada ya kingine. Kwa mfano.

28. Alisoma akachoka akalala
29. Alikwenda akafika
30. Alikula akamaliza

Aspekti hii hutumika katika mazingira ya njeo ya wakati uliopita.

Njeo inaweza kutambulishwa kwa kutumia kiambishi fulani cha njeo au isitambulishwe. Njeo pia inaweza kuonyeshwa na kiambishi cha kutambulisha aspekti. Vyovyote iwavyo

kila kitenzi kisaidizi lazima kiwe na njeo au aspekti.

3.0.1.2 Modali

"Katika uamilifu wake kiutambuzi modali huhusisha tukio na ukweli katika mazingira tofauti; mazingira mbapo tamko ni la kweli (tendi), huenda likawa kweli (chaguo), linaweza kuwa kweli (uwezekano), lazima liwe kweli (kuhitajika) n.k."

(Tafsiri yetu)

(Stockwell, R. P. 1977: ? )

Katika lugha ya kiswahili kuna modali zifuatazo:

- kwisha
- Kwenda
- Pata
- kuja
- weza
- taka
- kuwa
- lazimika
- bidi
- ngali

Tukirudia, sheria ya kitenzi kisaidizi ni kama ifuatavyo:

TS ⟶ njeo + (modali) + (me) + (kuwa) + (KI)

Njeo inaweza kufuatwa na moja, baadhi au zote za kategoria za maneno zilizopo. Katika mifano ya vitenzi ambavyo tumekwisha kuviona, kila kimoja kilikuwa na njeo ambayo ilisimamia mahali pa kisaidizi.

Ili kurahisisha mpangilio, kila sehemu ya TS tutaipa herufi yake kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| nj | - | A |
| m | - | B |
| me | - | C |
| kuwa | - | D |
| ki | - | E |

Kutokana na sheria hii ya kitenzi kisaidizi tunaweza kupata ruwaza kumi na nne za TS kama ifuatavyo:


TS → A
→ A + B
→ A + C
→ A + D
→ A + E*
→ A + B + C
→ A + B + D
→ A + B + E
→ A + B + C + D
→ A + B + C + D + E
→ A + C + D
→ A + C + E
→ A + C + D + E
→ A + D + E

Baadhi ya ruwaza hizi ziko makosa kisarufi. Baadhi yake zikifuatiwa na kategoria fulani za maneno zinakuwa sahihi kisarufi lakini haziwezi kufuatiwa na kitenzi. Sheria ya

kitenzi kisaidizi ni kwamba ni lazima kifuatiwe na kitenzi kikuu. Kama ruwaza ya kitenzi kisaidizi haiwezi kufuatiwa na kitenzi basi ruwaza hiyo si sahihi. Tutachunguza ruwaza moja baada ya nyingine hapo chini.

3.0.1.3 TS ⟶ A / TS ⟶ nj

Katika ruwaza hii sentensi huwa na kitambulishi cha njeo au aspekti bila kuwa na modali wala-me- wala kuwa, wala ki. Mfano wa kielelezo tungo ni kama ufuatavyo.




31. ⇒ Mti ulianguka


Kiambishi cha kiima huzalishwa katika KN na huletwa kwenye KT na kuambishwa nyuma ya kiambishi cha njeo.

Wakati mwingine njeo inaweza isitambulishwe. Kwa mfano pale ambapo kitambulishi cha aspekti ya kukamilika kwa jambo -me- kimetumiwa, au katika sentensi ya kuwa, au ya kuwa na ya njeo ya wakati uliopo. Kwa mfano:


32 Kache ni mgonjwa

33. Dama hana kalamu

Katika sentensi 32 kitenzi kikuu ni 'ni' na pia arki ya jeo imo katika kitenzi kikuu hicho. Kielelezo tungo chake ni kama kifuatavyo.




Katika sentensi 33 kitenzi kikuu ni kuwa na. Sentensi hii hata hivyo ni kanushi. Njeo ni ya wakati uliopo lakini haitambulishwi. Kielelezo tungo cha sentensi hii ni kama kifuatavyo:



3.0.1.4 TS ⟶ A + B / TS ⟶ nj + m

Sheria hii inasema kitenzi kisaidizi kina muundo wa njeo na modali. Muundo huu unapaswa kufuatiwa na kitenzi kwa sababu modali inatakiwa kuarifu ukweli fulani kuhusu kitenzi kikuu. Katika muundo huu kitenzi kikuu huwa kitenzi kisoukomo. Mifano ni kama ifuatavyo:

34. Ayubu ataweza kucheza

KN nj m T(kisoukomo)


N

35. Sote tulitaka kuangamia baharini

KN nj m T (Kisoukomo) EM

V

Kilelezo tungo cha sentensi 35 ni kama kifuatavyo:




⟹ Sote tulitaka kuangamia baharini.

Inaweza kudaiwa kwamba tulizoziita modali hapa si modali hasa bali ni vitenzi lekezi ambavyo hujalizwa na vitenzi visoukomo. Kile ambacho tumekichukulia kuwa kitenzi kikuu hapa kinachukuliwa kuwa ni yambwa ambayo uamilifu wake wa kisintaksia ni kijalizo. Mitazamo yote miwili iko sahihi.


Modali 'huenda' huwa haichukui viambishi vyovyote. Modali hii inapotumiwa katika muundo huu, kiambishi cha njeo hutambulishwa katika kitenzi kikuu. Kwa mfano:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 37. | Yesu | huenda | a ta | fufuka |
| | KN | m | nj | T |
| | N | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 38. | Marehemu | huenda | a li | kula | sumu |
| | KN | m | nj | Tl | KN |
| | N | | | | N |

3.0.1.5 TS ⟶ A + C / TS ⟶ nj + me

Sheria hii inasema kuwa kitenzi kisaidizi huwa na muundo wa njeo pamoja na 'me'. Sheira hii inaingiliana na sheria TS ⟶ nj kwa sababu 'me' ni kitambulishi cha aspecki ya kukamilika kwa tukio au kitendo; na kiambishi hiki pia hionyesha njeo ya wakati uliopita. Kielelezo tungo kifuatacho kitasaidia kuonyesha hali hii.




39 ⟹ Kamau ameiba pesa

Kisaidizi kinachoonyeshwa na sheria hii ni njeo na aspekti tu, mifano zaidi ni kama ifuatavyo:

40. Maria amepika samaki


41. Mtoto amenunua kalamu

42. Mzee ameoa

3.0.1.6 TS ⟶ A + D / TS ⟶ nj + kuwa

Sheira hii inasema kuwa kitenzi kisaidizi kinaweza kuwa na muundo wa nj na kuwa. Kuwa inaweza kutumika kama kitenzi kishirikishi katika sentensi shirikishi. Kitenzi kishirikishi hiki kinapotumiwa katika njeo ya wakati uliopita au njeo ya wakati ujao hutumika kama kitenzi kikuu ambacho huchukua viambishi vya njeo, viambishi vya ukubaliano wa kiima n.k. kwa mfano:

43. Sidi alikuwa mwoga




Katika mazingira haya sheria hii iko makosa. Kitenzi kishirikishi kuwa si sehemu ya kitenzi kisaidizi bali ndicho kitenzi kikuu.


Kitenzi cha kuwa (kitenzi kishirikishi) kinapotumika katika njeo ya wakati iliopo, kwa mfano katika sentese zifuatazo.

44. Mti huu ni mrefu

45. Katisa ni mchafu

46. Wale wanafunzi si hamsini;

Kitenzi kishirikishi hiki huwa ndicho kitenzi kikuu. Kitenzi hiki pia huonyesha ngeli ya wakati uliopo ambayo haitambulishwi. Tazama kielelezo tungo kifuatacho:




⟹ Mti ule ni mrefu.

Kielelezo tungo hiki kinaonyesha kuwa njeo haikutambulishwa. Njeo imebebwa katika kitenzi kikuu. Kwa kuwa njeo imo katika kitenzi kikuu tunaweza kudai kuwa katika mazingira kama haya sheria hii iko sahihi.

.0.1.7 TS ⟶ A + E / TS —— nj + ki*

Sheria hii inasema kuwa kitenzi kisaidizi kina muundo wa njeo na ki. Kama ambavyo tumekwisha kuona 'ki' ni kiambishi ambacho huonyesha aspekti ya kuendelea kutendaka au kutukia kwa kitendo au tukio linalohusika. Katika sarufi ya lugha ya kiswahili hakuna muundo kama huu. Sheria hii basi iko makosa. Sheria hii ingezalisha miundo isiyo sahihi kama ifuatavyo:

47. Ayoti alikicheza vizuri*
48. Kanze alikiimba*
49. Kahaso amekilala*

3.0.1.8 TS ———→ A + B + C/TS———→ nj + m + me

Sheria hii inasema kuwa kitenzi kisaidizi huwa na muundo wa njeo, modali na 'me'. Muundo huu wa kitenzi kisaidizi hufanya kazi sawa na ule wa sheria TS———→ nj + m. Tofauti ya pekee ni kwamba muundo huu una kitambulishi cha aspekti ya kukamilika kwa kitendo au tukio -me. Njeo katika muundo huu ambayo ni njeo ya wakati upiopita, hubebwa na kiambishi cha aspekti 'me'. Kama katika sheria TS———→ nj + m, modali hufuatwa na kitenzi kisoukomo isipokuwa modali 'huenda'. Modali huenda kama ambavyo tumekwisha kutaja haichukui viambishi vyovyote. Modali hii hufuatwa na modali nyingine ambayo ndiyo inayochukua 'me' na viambishi vingine. Mifano ya miundo yenye modali mbali na huenda ni kama ifuatavyo;

50 mama ameweza kufika mapema

KN me m T(Kisoukomo E )wakati)

N

51. Mnazi umekuja kutatwa

KN me m T (kisoukomo)

N

52 Babu amekwisha kufa

KN me m T(Kisoukomo)

N

Mifano ya miundo yenye modali huenda ni kama ifuatavyo:

53. Amina huenda amepata kumwona

KN m me m T(Kusoukomo)
N


54. Saidi huenda amewesa kulipa

KN m me m T(Kisoukomo)
N

55. Mgeni huenda ametaka kupotea

KN M me M T (kisoukomo)
N

Mfano wa kielelezo tongo kuonyesha muundo huu ni kama ufuatavyo.




⟹ Saidi huenda ameweza kulipa.

Modali huenda inaweza kufuatwa na modali nyingine yoyote. Modali zote mbili hufanya kazi kama shada kuonyesha ukweli fulani kuhusu kitenzi kikuu, ingawa kila moja huonyesha ukweli tofauti.

3.0.1.9 TS ⟶ A + B + D / TS ⟶ nj + m + kuwa

Sheria hii inasema kuwa Kitenzi kisaidizi kinaweza kuwa na muundo wa njeo pamoja na modali pamoja na kuwa. Katika muundo huu kitambulishi cha njeo huambishwa nyuma ya kuwa kama njeo inyohusika ni ya wakati uliopita au ni ya wakati ujao. Mifano ni kama ifuatavyo:

56. Babu alikuwa anaweza kusoma

KN nj kuwa m T (kisoukomo)
N

57. Sisi tutakuwa tungali kuandika

KN nj kuwa m T (kisoukomo)
N

58. Kiti changu kilikuwa kinataka kuvunjika

KN
N kim nj kuwa m T (kisoukomo)

Kama ambavyo inaonekana katika sentensi hizi, kuwa huja kabla ya modali. Katika mazingira haya sheria hii tunaweza kuiandika upya kuwa TS ⟶ nje + kuwa + m.

Muundo huu wa kitenzi kisaidizi unaweza kuwa na ruwaza zifuatazo:

TS ⟶ huenda + kuwa + (nj + (T))

TS ⟶ weza + kuwa + (nj + (T))

Mabano - ( ) yanaonyesha kuwa arki zilizofungiwa hutokea pamoja kama neno moja. Lazima ifahamike kuwa kitenzi katika mabano si sehemu ya kitenzi kisaidizi. Tulichotaka kuonyesha ni kwamba kitambulishi cha njeo huambishwa kwenye kitenzi kikuu. Mifano ya ruwaza hizi ni kama ifuatavyo:

59. Katana huenda akawa anasoma

60. Shangazi huenda akawa atakuja

61. Nanasi laweza kuwa liliiva

3.3.1.10 TS ⟶ A + B + E/TS ⟶ nj + m + ki*


Sheria hii inasema kwamba kitenzi kisaidizi kina muundo wa njeo pamoja na modali pamoja na ki. Muundo kama huu haupatikani katika sarufi ya kiswahili. Miundo isiyokuwa sahihi kisarufi inayoundwa na sheria hii ni kama ifuatavyo:

63. Juma aliweza akiimba*

64. Mti huenda ukianguka*

3.0.1.11 TS ⟶ A + B + C + D/TS ⟶ nj+ M + Me + kuwa

Sheria hii inasema kuwa kitenzi kisaidizi kina muundo wa njeo na modali na 'me' na kuwa. Modali ikiwa 'huenda ruwaza huwa kama ilivyo katika kielelezo tungo kifuatacho:




65. ⇒ Karisa huenda alikuwa amelewa

Baada ya ugeuza maumbo, muundo huu huchukua ruwaza ifuatayo:

TS ⟶ Huenda + njeo + kuwa + me

Mifano zaidi ya miundo yenye ruwaza hii ni kama ifuatavyo:

66. Huenda akawa amelewa

67. Gari huenda litakuwa limeharibika

68. Nguo yangu huenda itakuwa imeraruka

Kama invyoonyeshwa katika sheria badalia, kitambulishi cha njeo huambishwa kwenye kuwa na me huambishwa kwenye kitenzi kikuu.

Sheria hii pia inaweza kuchukua ruwaza ifuatayo

TS ⟶ nj + m + kuwa + [Me + (T)]

Mabano- [ ] yanaonyesha kuwa kilivyomo huunda neno moja, na duara ⬭ linaonyesha kuwa kilichomo si sehemu ya kitenzi kisaidizi. Katika ruwaza hii kitambulishi cha njeo huambishwa kwenye modali na me huambishwa kwenye kitenzi kikuu. Mifano ya muundo huu ni kama ifuatavyo:

69. Anapaswa kuwa amefika
70. Kinaweza kuwa kimepotea
    Tulikwisha kuwa tumekaribishwa


3.0.1.12 TS ⟶ A + B + C + D + E /

TS ⟶ nj + m + me + kuwa + ki

Kwa mujibu wa sheria hii kitenzi kisaidizi kina muundo wa njeo na modali na me na kuwa na ki. Hii ndiyo ruwaza ndefu zaidi ambayo TS cha kiswahili kinaweza kuchukua. Mifano ya sentensi zenye muundo huu wa TS ni kama ifuatavyo

71. Mama huenda amekuwa akipika
72. Mwalimu huenda amekuwa akiandika barua
73. Mohammed awezekana amekuwa akifunga
74. Kunaweza kuwa kumekuwa kukinyesha
75. Mgema aweza kuwa amekuwa akipanda mnazi.

Katika muundo huu njeo huwa haitambulishwi. Njeo hubebwa na me. Njeo hii huwa ya wakati uliopita. Kiambishi cha aspekti ya kukamilika - kwa kitendo au tukio - me- huambishwa kwenye kuwa. Kiambishi ambacho hutambulisha aspekti ya kuendelea kutendeka au kutukia kwa kitendo au tukio ki huambishwa kwenye kitenzi kikuu. Tazama kielelezo tungo kifuatacho:




⟹ Mama huenda amekuwa akipika

Modali weza na kuwa zinaweza kutumiwa pamoja kama shada kitenzi kuonyesha ukweli fulani wa kitenzi kikuu. Mfano wa matumizi haya umo katika sentensi zilizopo hapo juu.

3.1.1.13. TS ⟶ A + C + D / TS ⟶ nj + me + kuwa


Sheria hii inasema kitenzi kisaidizi huwa na njeo pamoja na me pamoja na kuwa. Muundo huu huwa wa sentensi za kuwa au sentensi shirikishi ambazo njeo yake huwa ya wakati uliopita, na zenye aspekti ya kukamilika kwa kitendo au tukio. Mifano ya sentensi zenye kitenzi kisaidizi chenye muundo huu ni kama ifuatavyo:

76. Mwanafunzi amekuwa mgonjwa

77. Kitabu kimekuwa kikuukuu

78. Mchungwa umekuwa tasa

Mfano wa kielelezo tungo ni kama ufuatavyo:




⇒ Kitabu kimekuwa kikuukuu.

3.0.1.14 TS ⟶ A + C + E / TS ⟶ nj + me + ki*

Sheria hii inasema kuwa kitenzi kisaidizi kina muundo wa njeo pamoja na me pamoja na ki. Katika sarufi ya kiswahili hakuna muundo kama huu. Sheria hii iko makosa kwa sababu haiwezi kuzalisha muundo ulio sahihi kisarufi. Sentenzi zisizokuwa sahihi zinazoweza kuzalishwa na sheria hii ni kama zifuatavyo:


79. Mtoto ame kicheka mpira*
80. Mzee amekilala fofofo*
81. Mgonjwa amekikufa*

3.0.1.15 TS ——→ A + C + D + E / TS ——→ Nj + me + kuwa + ki

Kulingana na sheria hii kitenzi kisaidizi kina muundo wa njeo na 'me' na 'kuwa' na ki. Sheria hii huzalisha sentensi zenye kitenzi kishirikishi au kitenzi cha kuwa na ambazo njeo yake ni ya wakati uliopita. Aspekti ni ya kukamilika kutendeka au kutukia. Kitambulishi cha aspekti hii - me- huambishwa kwenye kitenzi cha kuwa. Kitambulishi cha aspekti ya kuendelea kufanyika au kutukia - ki - huambishwa kwenye kitenzi kikuu. Mifano ya sentensi zenye TS chenye muundo huu ni kama zifuatavyo;

82. Mtoto amekuwa akicheza mpira
83. Mzee amekuwa akilia sana
84. Waumini wamekuwa wakiomba kanisani

Mfano wa kielelezo tungo cha kuonyesha muundo huu ni kama ufuatavyo:




⟹ Mzee amekuwa akilia sana

3.0.1.16 TS ⟶ A + D + E / TS⟶nj + kuwa + ki

Sheria hii inaonyesha kuwa kitenzi kisaidizi kinaweza kuwa na muundo wa njeo na kuwa na ki. Sheria hii huzalisha sentensi shirikishi au sentensi zenye kitenzi cha kuwa na ambazo huwa na kitenzi chenye aspekti ya kuendelea kufanyika kwa kitendo au kutikia kwa tukio linalihisika. Kiambishi cha aspekti - ki- hutumiwa katika sentensi zenye njeo ya wakati uliopita na njeo ya wakati ujao hali kiambishi -na- au -a- hutumiwa katika sentensi zenye njeo ya wakati uliopo. Mifano ya sentensi zenye TS chenye muundo huu ni

kama ifuatavyo;

85. Magari yatakuwa yakipita


86. Fundi alikuwa akijenga nyumba

87. Mkoba ulikuwa ukiraruka

88. John akawa anakula

89. Hamisi andiye anayesema

Mfano wa kielelezo tungo wa kuonyesha muundo huu ni kama ufuatavyo:




⟹ Magari yatakuwa yakipita

4.0 SURA YA NNE

4.0.1 KITENZI KISAIDIZI KATIKA MASWALI

4.0.1.1 Utangulizi

Katika sura hii tutachunguza tabia ya kitenzi

kisaidizi katika sentensi maswali katika lugha ya kiswahili. Kuna aina mbili kuu za maswali; kuna maswali ambayo yanatarajia majibu ya maelezo na maswali ambayo maswali ambayo hutarajia jibu la ndiyo au la.

Maswali ambayo hutarajia majibu ya maelezo huwa na vipashio maalumu ambavyo hufanya kazi ya kuuliza. Vipashio hivi kwa mujibu wa kazi hii tutaviita viulizi. Kiswahili kina viulizi vifuatavyo.

| | |
|---|---|
| Nani<br>Nini<br>Gani<br>-pi | Mtu au kitu |
| Namna gani<br>vipi<br>-je | Jinsi |
| Kwa nini<br>mbona | Sababu |
| Lini | wakati |
| -ngapi | idadi |
| wapi | mahali |

Viulizi -pi na -ngapi ni mizizi ambayo huhitaji kuambishwa. Kiulizi -pi huambishwa na kitambulishi cha kima; kwa mfano:

Kiti kipi?

Mti upi?

Kalamu ipi?

hali kiulizi -ngapi huambishwa na kitambulishi cha nomino; kwa mfano:

Watu Wangapi?

Viti vingapi?

Meno Mangapi?

Kiulizi -je kiko katika umbo la kiambishi ambacho huambishwa mwishoni mwa kitenzi; kwa mfano:

kalamu ilivunjikaje?

Pesa zilipoteaje?

Kisu kilikukataje?

Kabla ya swali kipashio ambacho si cha lazima 'Je' huwekwa. Kipashio hiki si kiulizi bali hutahadharisha au hutanguliza kwamba sentensi hiyo ni ulizi.

Tutatumia sentensi zifuatazo ambazo tayari tumekwisha kuzitumia kwa mahitaji mengine kama vielelezo katika ufafanuzi:

31. Mti ulianguka

32. Kache ni mgonjwa

34. Ayubu ataweza kucheza

37. Yesu huenda atafufuka
38. Kamau ameiba pesa
52. Babu amekwisha kufa
54. Babu huenda ameweza kulipata
56. Babu alikuwa anaweza kusoma
65. Karisa huenda alikuwa amelewa
71. Mama huenda amekuwa akipika
76. Mwanafunzi amekuwa mgonjwa
82. Mtoto amekuwa akicheza mpira
85. Magari yatakuwa yakipita

Tutagawanya maswali katika makundi mawili; maswali yenye viulizi na maswali yasiyo viulizi. Maswali yenye viulizi ni yale yenye kuhitaji majibu ya maelezo na maswali yasiyo viulizi ni yale yanayotarajia jibu la ndio au la.

Uchunguzi huu wa tabia ya kitenzi kisaidizi katika maswali utatuwezesha kuona ruwaza mbali-mbali ambazo kitenzi kisaidizi kinaweza kuchukua katika mazingira tofautitofauti

4.0.1.1 Kitenzi kisaidizi katika maswali yenye viulizi

Isipokuwa kiulizi -je ambacho lazima kiwe katika KT, viulizi vyote huwa katika KN. Wakati mwingine kiulizi kinaweza kuwa kipashio cha pekee katika KN; kwa mfano:

FOR USE IN THE LIBRARY ONLY


UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

1. Mbona alikula sumu?
KN nj T KN
Kiulizi N

2. Nini kimeanguka ?
KN me T
Kiulizi

3. Nani alisahau ?
KN nj T
Kiulizi

Kielelezo tungo cha sentensi 1 ni kama kifuatavyo




Sentensi msingi ya sentensi 1 ni Alikula sumu

Sentensi 1 imefikiwa baada ya ugeuza maumbo wa swali.

Sentensi zenye kiulizi zinaweza kuwa na ruwaza zifuatazo:

S ⟶ N + Kiulizi + TS + T + (KN, KE, KH)

S ⟶ N + TS + T + (KN, KE, KH) + Kiulizi

S ⟶ Kiulizi + N + TS + T + (KN, KE, KH)

S ⟶ TS + T + (KN, KE, KH) + KN

S ⟶ N + Kiulizi + TS + T + (N, KE, KH)

Katika ruwaza hii sentensi huwa na nomino ikifuatiwa na kiulizi kikifuatiwa na kitenzi kisaidizi kikifuatwa na kitenzi kikuu ambacho kinaweza kufuatwa na kundi vumishi au kundi elezi au kundi husishi. Kwa mfano sentensi

3. Mti ulianguka, inaweza kuwa

| mti | upi | Uli | anguka ? |
|---|---|---|---|
| KN | Kiulizi | nj | T |
| N | | | |

| Mti | gani | uli | anguka ? |
|---|---|---|---|
| KN | Kiulizi | nj | T |
| N | | | |

4.0.1.1.1 SW ⟶ KN + TS + T + (KN,KE,KH) + Kiulizi

Sheria hii inaonyesha kuwa swali huwa na nomino, ikifuatwa na TS kikifuatwa na T ambacho kinaweza kufuatwa na KN au KE

au KH ambalo hufuatwa na kiulizi kwa mfano:

Mti ulianguka vipi ?

KN nj T Kiulizi

N

Mti ulianguka lini ?

KN nj T Kiulizi

N

Mti ulianguka wapi ?

KN nj T Kiulizi

N

4.0.1.1.2 SW ⟶ Kiulizi + KN + TS + T + (KN, KE, KH)

Kulingana na sheria hii swali linaweza kuwa na muundo wa kiulizi kikifuatwa na KN likifuatwa na TS kikifuatwa na T ambacho kinaweza kufuatwa na KN au KE au KH. Kwa mfano:

TS

Kwa nini babu huenda ameweza kulipata ?

Kiulizi KN m Me m T

N

4.0.1.1.3 SW ⟶ TS + T + (KN + KE + KH) + KN

Sheria hii inasema swali lina muundo wa

TS kikifuatwa na T ambacho kinaweza kufuatwa na KN au KE au KH likifuatwa na KN. Kwa mfano;

Ulianguka vipi Mti ?
nj T Kiulizi KN

4.0.1.2.4 NI + Kiulizi na kitenzi kisaidizi chenyw modali

Katika mifano yote hapo juu mpangilio wa KT haukubadilishwa; umebaki kama ulivyo katika sentensi msingi. Mpangilio wa kitenzi kisaidizi hata hivyo unaweza kutatizwa au kubadilishwa katika baadhi ya maswali yenye viulizi.

Mahali pa kwanza ambapo ruwaza ya TS inaweza kubadilika ni katika ruwaza

S ⟷ Kiulizi + KN + TS + T + (KN, KE, KH)

Pale ambapo kiulizi kinatangulia katika sentensi kipashio ni hutumiwa kabla ya kiulizi. Kwa mfano;

37. Ni kwa nini huenda yesu atafufuka

39. Ni nani aliyeiba pesa

34. Ni namna gani Ayubu ataweza kucheza

Kipashio ni "ni" sura ya kitenzi cha kuwa katika njeo ya wakati uliopo. 'Ni' katika mazingira haya bado inaonyehsa njeo ya wakati uliopo ya swali linaloulizwa. Njeo ya kitenzi inaweza kuwa tofauti. kwa mfano katika sentensi 37, njeo ya kitenzi ni ya wakati ujao. Kiulizi mbona hata hivyo hakiwezi kutanguliwa na ni.

Mpangilio wa kitenzi kisaidizi pia unaweza kugeuka kama TS hicho kina modali. Nomino inaweza kuwekwa baada ya modali, na pia modali inaweza kuwekwa kabla ya kiulizi. Mifano ni kama ifuatavyo:

54. Babu kwa nini huenda ameweza kulipata ?

KN kiulizi m me m T

N

Kwa nini huenda babu ameweza kulipata ?

Kiulizi m KN me m T


N

Sentensi msingi ya maswali haya ni kama ifuatavyo;

54. Babu huenda ameweza kulipata

Baada ya ugeuzamaumbo wa swali kutokea ndipo tunapata maumbo ya maswali yaliyo hapo juu.

Kielelezo tungo cha maswali haya baada ya ugeuzamaumbo wa swali kutokea ni kama kifuatavyo;



### 4.0.1.2 KITENZI KISAIDIZI KATIKA MASWALI YASIYO KIULIZI

Kama tulivyosema swali lisilo kiulizi ni swali ambalo linatarajia jibu la ndio au la. Kila sentensi ya kiswahili inaweza kuwa swali endapo kiimbo chake kitageuzwa kiwe cha kupanda.


31 Mti ulianguka ?

37 Yesu huenda atafufuka ?

52. Babu amekwisha kufa ?

Umbo ndani la maswali haya huwa sawa na lile la sentensi yenye dhamira arifu isipokuwa katika swali kutoka kifundo cha sentensi hu

Kwa mfano;



Sentensi iwapo na mauundo huu husomwa kwa kiimbo cha kupanda na hivyo kuipa uamilifu mpya kama swali.

Sentensi ya kiswahili isiyo kiulizi inapopitia mfanyiko wa ugeuzamaumbo wa swali huwa haiongezwi vipashio vingine vyovyote. Kama tulivyokwisha kuona hata hivyo, kiimbo hubadilika na kuwa cha kupanda. Mpangilio wa vipashio vya sentensi pia unaweza kugeuka. Ruwaza zifuatazo zinaweza kupatikana katika sentensi swali.

SW ⟶ KN + KT

SW ⟶ KT + KN

SW ⟶ M + KN + nj + (me) + (kuwa)+(KI)+) T(KN,KE,K

SW ⟶ M + Kuwa + nj + (me) + T(KN,KE,KH) + KN

SW ⟶ M KN + Kuwa + nj + (me) + T

4.0.1.2.1 SW ⟶ KN + KT


Sheria hii inasema swali lina muundo wa KN likifuatwa na KT. Maelezo na mifano ya sheria hii ni kama tulivyokwisha kueleza hapo juu.

4.0.1.2.2 SW ⟶ KT + KN

Sheria hii inasema swali lina muundo wa KT Likifuatwa na KN Kiswahili kinaruhusu sentensi ya kawaida kuwa na muundo huu. Kwa mfano

Amekwisha kufa babu.

Sentensi ya muundo huu ili iweze kuwa swali inapaswa kuwa na kiimbo cha kupanda. Kiimbo ndicho ambacho huamua kama ni swali au ni sentensi arifu. Kielelezo tungo cha kueleleza umbo hili ni kama kifuatavyo




⟹ Kiimbo cha kupanda

Katika sarufi ya kiswahili vitenzi vyenye silabi moja huchukua kiwakilishi cha kitenzi kisoukomo - ku- wakati kinapotumika katika sentensi. Sheria hii hugeuza umbo la kitenzi fa na kuwa kufa.

4.0.1.2.3 SW ⟶ M + KN + nj +(me) +(Kuwa)+(KI)+T+KN,KE,KH)

Sheria hii inasema kuwa swali lina muundo wa modali ikifuatwa na kundi nomino likifuatwa na njeo au aspekti ya utimilifu ikifuatwa na kuwa ambayo inaweza kufuatwa na aspekti ya kuendelea ikifuatwa na kitenzi kikuu ambacho kinaweza kufuatwa na kundi nomino au kundi elezi au kundi husishi. Mabano ( ) yanasema kwamba vipashio vilivyomo vinaweza kuwepo au visiwepo . Mifano ni katika vielelezo vifuatavyo;

```
                                                    N
                                               H    KN
Huenda  mama  alikuwa  akipika  nyama  kwa  stovu
m       KN    nj kuwa  KI  T    KN     KH
        N                       N
```

```
                                        Vh      VK
                               N           KV
Huenda  maria  alikuwa  akiimba  wimbo  mzuri  sana
M       KN     nj kuwa  ki  T           KN
        N
```

Katika umbo hili TS kimetapanywa kwa kuingizwa KN katikakati ya modali na njeo au kuwa.

4.0.1.2.4 SW ⟶ M + Kuwa + nj+(me)+(ki)+T(KN,KE,KH)+KN

Sheria hii inasema swali lina umbo la modali ikifuatwa na kuwa ikifuatwa na njeo ambayo yaweza kufuatwa na aspekti ya utimilifu ikifu-fuatwa na kitenzi kikuu ambacho kinaweza kufuatwa na kundi nomimno au kundi elezi au kundi husishi likifuatwa na kundi nomino. Mifano ni kama ifuatavyo;

Vh Vk
N KV
Aweza kuwa amechimba shimo refu sana panya?
M kuwa me T KN KN
N

4. Aweza kuwa amekuwa akindesha gari polepole sana.
m me kuwa ki T KN KE
N
Eh EK

Josefu ?
KN
N

4.0.1.2.5 SW ⟶ M + KN+ Kuwa + nj+(me)+T+(KN,KE,KH)

Sheria hii inasema swali linaweza kuwa na umbo la modali ikifuatwa na kundi nomino likifuatwa na njeo ambayo inaweza kufuatwa na aspekti ya utimilifu ikifuatwa na kitenzi

kikuu ambacho kinaweza kufuatwa na kundi nomino au kundi elezi au kundi husishi.

Sheria hii kwa kweli ni sehemu ya sheria SW M+KN+nj+(me)+(kuwa)+KI+T+(KN,KE,KH)

Lakini tumeitoa peke yake kwa madhaumuni ya kurahisisha maelezo. Kwa mfano:

5. Yaweza gari kuwa imeharibika

| Yaweza | gari | kuwa | ime | haribika |
|---|---|---|---|---|
| m | KN | kuwa | me | T |
| | N | | | |

6. Huenda mgeni akawa alipotea mjini ?

| Huenda | mgeni | akawa | ali | potea | mjini |
|---|---|---|---|---|---|
| M | KN | kuwa | nj | T | KE |
| | N | | | | EM |

Tumeona kwamba TS kinaweza kuchuakua ruwaza tofauti katika maswali yasiyo kiulizi. Ubadilishaji nafasi huu wa vipashio vya TS hutokana na umulikaji, kile ambacho msemaji anataka kumulika.

# 5.0 SURA YA TANO

## 5.1 Hitimisho

Katika utafiti huu tumeona kwamba kitenzi kisaidizi cha kiswahili huchukua njeo, modali, aspekti ya utimilifu, aspekti ya kuendelea na kitenzi cha kuwa. Tumeona pia kwamba modali za kiswahili zinaweza kutumiwa peke yake kama kitenzi kikuu cha sentensi. Katika matumizi kama hayo modali hizi huwa uamilifu wake si kama modali bali kitenzi kikuu.

Tumeona kwamba katika kiswahili kuna njeo tatu, njeo ya wakati uliopo, ya wakati uliopita na wakati ujao. Njeo hizi hutambulishwa kwa kutumia vitambulishi maalumu. Njeo hata hivyo inaweza isitambulishwe katika sentensi. Njeo inaweza kubebwa na kitambulishi cha aspekti ya utimilifu. Kitambulishi cha njeo ya wakati uliopo kinaweza kudondoshwa na kuacha sentensi bila njeo. Itokeapo hivi huchukuliwa kuwa njeo ni ya wakati uliopo na pia kitenzi hicho kinaonyesha kitendo ambacho ni tabia au kazi ya mtenda.

Kundi nomino huzalisha baadhi ya vipashio vya kitenzi kisaidizi au kundi tenzi kwa ujumla.

Vitambulishi vya ukubaliano wa kitenzi na nomino huzalishwa kwenye kundi nomino. Vipashio hivi ni kitambulishi cha ngeli au nomino;kitambulishi cha kiima na kitambulishi cha yambwa. Vitambulishi hivi huzalishwa kwenye nomino na kwa sheria ya ugeuzamaumbo wa ukubaliano huvushwa kwenye kundi tenzi na kuambishwa kwenye kitenzi na/au kisaidizi. Sarufi geuzamaumbo zalishi hata hivyo hapa ina upungufu maana haituonyeshi wazi ni vipi arki hizi zilizozalishwa kwenye kundi nomimno huenda kwenye kitenzi.

Utafiti huu umetuonyesha kwamba kitenzi kisaidizi huzalishwa katika umbo ndani la sentensi. Kwa kuwa Kiswahili ni lugha ambishibainishi baadhi ya visaidizi vya kitenzi huambishwa pamoja. Ugeuzamaumbo wa ukubaliano, wa ukanushi,wa swali, nk huzalisha umbo nje la sentensi,kitenzi kisaidizi kikiwemo.

Uchunguzi huu umetuonyesha kuwa vipashio vya kitenzi kisaidizi ispokuwa modali huwa ni viambishi. Hali hii pengine inatokana na kwamba kiswahili ni lugha ambishi baininshi.

Tumeona kwamba modali za kiswahili huchukua viambishi awali sawa na vile vya kitenzi kikuu lakini modali 'huenda' haichukui viambishi vyovyote hata vile vya kuonyesha ukubaliano na nomino au kundi nomino.

Katika sentensi za kuwa na zenye kitenzi chenye njeo ya wakati uliopo, njeo huwa haitambulishwi; njeo hubebwa tu na kitenzi cha kuwa ambacho ndicho kitenzi kikuu.

Tumepata kwamba baadhi ya modali huwa na utata katika uamilifu wake kama vitenzi visaidizi. Modali hizi kisintaksia huonekana tu kama vitenzi elekezi na kile ambacho huwa kitenzi kikuu kinachosaidiwa na modali hii huonekana kama kijalizo. Hali hii huonekana sana pale ambapo kitenzi kikuu ni kitenzi kisoukomo. Uamilifu wa modali hizi kama modali hupata nguvu tukitumia kigezo cha kisemantiki. Pengine nadharia zingine zitaweza kueleza hali hii na kuondoa utata uliopo.

Tumeona kwamba nadharia ya sarufi geuzamaumbo zalishi imeweza kueleza vizuri kitenzi kisaidizi cha kiswahili. Upungufu wa nadharia hii tulioona ni kule kutoweza kueleza wazi namna vipashio vya ukubaliano wa nomino vinavyoenda kutoka kundi nomino hadi kwenye kundi tenzi.

MAREJELEO

Ashton, E.O. (1944). Swahili grammar - including Intonation, London: Longman

Akmajian, A. and Heny, F. (1975). An introduction to the principles of transformational Syntax, The MIT press

Aurbach, J. Et-al (1968). Transformational grammar Washington Educational research associates, inc

Bach, E. (1977) . Syntactic theory University of Massachusetts at Amherst and Hampshire college

Bamgbose, A. (1966). A grammar of Yoruba Cambridge University press

Bolinger, D and Sears, D.A. (1981). Aspects of Language third edition, Harcourt Brace Jovanovich, inc

Chomsky, N. (1957) Syntactic Structures Mounton and co. N. V. publishers, the Hague

_______________ (1965). Aspects of the theory of syntax Massachusetts institute of technology

Huddleston, R. (1984). Introduction to the grammar of English cambridge University Press.

Jacobs, R. (1970). English transformational grammar Ginn and comapny Ltd.

Kapinga, M. C. (1983). Sarufi maumbo ya kiswahili Chuo Kikuu Cha Dar-es-salaam TUKI

Lester, M. (1971). Introductory transformational grammar of English,New York: Holt Rinehart and Winston.

Lyons, J. (1968). Introduction to theoretical Linguistics,Cambridge University press.

__________ (1970). Noam Chomsky The Viking press inc

Loogman, A(1965). Swahili grammar and synatax, Duquesne University press

Maw, J. (1969) Sentences in Swahili Gresham press

UNIVERSIT OF NA

Mbaabu, I (1985) Sarufi ya Kiswahili
Kenya publishing and book marketing Company Ltd.

Mdee, J.S. (1986) Kiswahili Muundo na matumizi yake
Nairobi: International publishers Ltd

Mgullu, R.S. (1990) The Struture of kiswahili sentences
M.A. thesis, University of Nairobi

Myachina, E.N. (1973) The Swahili language a descriptive grammar, London

Nkwera, .M.V. (1978) Sarufi na fasihi Sekondari na Vyuo, Dar-es-salaam: Tanzania publishing house.

Oke, D.O. ( ) On the construction and semantic interpretation of auxiliary clusters in Yoruba, in Bamgbose, A. ed. (1972) The Yoruba Verb Phrase, papers on the seminar on the Yoruba verb phrase, Ibadan 1-2 April, 1971

Owili, F.A. (1989) The Kiswahili verb phrase: A Syntactic analysis, M.A. thesis University of Nairobi.

Polome, E.C. (1967). Swahili language handbook Washington: Centre for applied Linguistics

Quirk, R. and Greenbaum, S. (1979). A University grammar of English, EBS edition UK: Longman.

Radford, A. (1988): Transformational grammar Cambridge University press.

Selby, N. (1987). Essential College English Second edition, Little, Brown and Company.

Stockwell, R. P. (1973). The major syntactic structures of English, Holt, rinehart and Winston, inc

_______________(1977) Foundations of Syntactic theory, New, Jersey: Prentice -Hall, inc

Thandi, C.G.(1988). Pronominalization in Kiswahili An approach to the binding theory, M.A. thesis University of Nairobi.

Tuki (1990) Kamusi sanifu ya isimu na lugha Dar-es-salaam

Vitale, A.J. (1981). *Swahili syntax*, New York

Watkins, M. H.(1937) *A grammar of Chichewa*, Linguistic society of America